USAID

KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI



2015-2019

# MKAKATI WA NCHI WA USHIRIKIANO WA KIMAENDELEO

Mageuzi ya Kijamii na ya Kiuchumi nchini Tanzania kuelekea Hadhi ya Nchi yenye Kipato cha Kati ifikapo mwaka 2025 Yameendelezwa

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| **AZAKI** | Asasi za Kiraia |
| **LeMa** | Lengo la Maendeleo |
| **MaKa** | Malengo ya Kati |
| **MMTATA** | Mpango Mkuu wa Takwimu Tanzania |
| **MUU** | Mpango wa Ufuatiliaji wa Utendaji |
| **UKIMWI** | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| **UNDP** | Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa |
| **USAID** | Shirika la Marekani la Misaada ya Maendeleo ya Kimataifa |
| **VVU** | Virusi vya UKIMWI |

2015-2019

# MKAKATI WA NCHI WA USHIRIKIANO WA KIMAENDELEO

Mageuzi ya Kijamii na ya Kiuchumi nchini Tanzania kuelekea Hadhi ya Nchi yenye Kipato cha Kati ifikapo mwaka 2025 Yameendelezwa

# Utangulizi

Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye uchumi unaokua kwa kasi kubwa sana barani Afrika. Kwa mujibu wa Benki ya Dunia, Pato la Taifa la kila mtu (*per capita GDP*) limeongezeka kutoka dola za Kimarekani 350 mnamo mwaka 2004 hadi dola za Kimarekani 998 mnamo mwaka 2014. Hata hivyo, umaskini uliokithiri bado unaendelea, asilimia 44 (2012) ya wananchi wa Tanzania wangali wakiishi chini ya mstari wa umaskini wa dola za Kimarekani 1.25 kwa siku. Kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa la Tanzania cha takriban asilimia 7 kwa mwaka, tangu mwaka 2000, kimekuwa haki¬onekani kwa Watanzania walio wengi (asilimia 73) wanaoishi viji¬jini. Ukuaji jumuishi na mpana1 (*Inclusive broad-based growth*) unak¬wamishwa na mambo mawili:

- **Ukuaji mdogo wa uzalishaji katika sekta zinazotegemea nguvu kazi shadidi** (*labor-intensive projects*) (kilimo kinaajiri aslimia 77 ya jumla ya ajira za taifa, lakini sekta hii ilikua kwa asilimia 4 tu katika muongo uliopita)
- **Kasi kubwa isiyobadilika, ya ongezeko la idadi ya watu.** Asilimia arobaini na nne ya Watanzania milioni 45 hivi sasa wana umri chini ya miaka 15. Kutokana na kasi ya hivi sasa ya ongozeko la idadi ya watu, inakisiwa kuwa ifikapo mwaka 2025, idadi ya watu nchini itafikia watu milioni 70.

Ifahamike kuwa, wanawake ni zaidi ya asilimia 50 ya idadi ya watu, hata hivyo, hali ya kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia inazidi kuendelea: kwa mfano, ujira wanaolipwa wanawake kwa wastani ni pungufu kwa asilimia 63 ukilinganisha na ule wanaolipwa wanaume, na wanawake wanapomiliki biashara, faida wanayozalisha ni pungufu kwa mara 2.4 ukilinganisha na ile inayozalishwa na wanaume.

Katika kipindi cha miaka mitano ya Mkakati huu wa Ushirikiano wa Kimaendeleo, Tanzania inayo fursa ya kutunga sera na kuendeleza uwekezaji utakaopunguza umaskini uliokithiri na kusukuma ma¬geuzi ya kijamii na kiuchumi kuelekea kwenye hadhi ya nchi zenye kipato cha kati. Mpango huu utafanikiwa kwa kuwawezesha wan¬awake na vijana; kuendeleza ukuaji jumuishi na mpana wa uchumi; na kuboresha utawala wa kidemokrasia, Tanzania inayo nafasi nzuri ya kufikia malengo yanayotarajiwa katika Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025 (*Development Vision 2025*), Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (*National Five Year Development Plan II*), pamoja na mikakati mingine ya kitaifa. Mkakati huu wa Ushirikiano wa Kimaendeleo unasaidia juhudi za Tanzania za kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii ya Watanzania; kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini; pamoja na kuendeleza utawala bora na uwajibikaji.

**Tanzania ni miongoni mwa nchi yenye uchumi unaokua kwa kasi kubwa sana barani Afrika.**

## Tanzania inayo nafasi nzuri ya kufikia malengo yanayo-tarajiwa katika Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025.

Tanzania ni nchi iliyo katika mstari wa mbele na mbia muhimu katika Mkakati wa Rais Obama wa kuziendeleza nchi zilizopo kusini mwa jangwa la Sahara. Wakiwa wabia wa karibu kwa zaidi ya miongo mitano, nchi za Tanzania na Marekani zinashabihiana kwa kuwa na dira moja ambayo inalenga kuinua ubora wa maisha ya Watanzania wote. Vipaumbele vya Serikali ya Marekani nchini Tanzania vinalenga yafuatayo:'

- **Kuendeleza serikali yenye uwazi na ya kidemokrasia** ambayo inaheshimu haki zote za binadamu;
- **Kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi ambayo ni endelevu na jumuishi**, yakiwemo matokeo chanya ya afya; na
- **Kuendeleza usalama na amani katika ngazi ya kanda.**

Shirika la Marekani la Misaada ya Maendeleo ya Kimataifa nchini Tanzania (USAID/Tanzania), likiwa kama shirika muhimu linaloshughulikia mambo ya nje, chini ya mamlaka ya Ubalozi wa Marekani uliopo Dar es Salaam, litaendeleza vipaumbele vilivyo katika Mkakati huu wa Ushirikiano wa Kimaendeleo.

Nadharia tete (*hypothesis*) ya mkakati huu ni kwamba: iwapo Tan¬zania itawawezesha wanawake na vijana, kuendeleza ukuaji wa uchumi ulio jumuishi na mpana, na kuimarisha utawala bora, ita¬fanikiwa kuleta mageuzi ya kijamii na kiuchumi kuelekea kuwa nchi yenye kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Kwa hakika, juhudi za kupunguza umaskini uliokithiri zitaweza kufanikishwa kwa kutumia rasilimali iliyosahaulika, yaani wanawake na vijana, na kwa kuweke za katika sekta muhimu za uchumi ambazo ni kilimo, maliasili, na nishati. Iwapo nadharia tete ya Mkakati huu itafanikiwa, Tanzania itasonga mbele na kufanikisha "moja ya matamanio makubwa adilifu," yanayojibu mwito wa kihistoria wa Rais Obama wa "kutokomeza umaskini uliokithiri ndani ya kipindi cha miongo miwili."



# Muktadha wa Maendeleo

Historia ya utulivu wa kisiasa na amani iliyopo hapa nchini baina ya makabila, pamoja na ukuaji endelevu wa uchumi katika miaka kadhaa iliyopita, kunaifanya Tanzania iwe nchi iliyobahatika kupata upendeleo wa kupokea msaada kutoka Marekani na wafadhali wengine. Tangu kuanzishwa kwa demokrasia ya vyama vingi mnamo mwaka 1992, Tanzania imeonyesha maendeleo thabiti katika kutetea demokrasia pamoja na kuheshimu haki za binadamu. Serikali ya awamu ya nne na ile iliyopo madarakani hivi sasa inaendeleza ajenda ya kukuza uchumi. Hata hivyo, Serikali ya Tanzania inakabiliwa na changamoto zisizoisha za umaskini katika eneo kubwa la nchi, vile vile miundombinu isiyotosheleza na ufisadi uliokithiri, ambavyo vinazuia ukuaji jumuishi wa kiuchumi.

Katika muongo uliopita, kumekuwa na maendeleo mazuri katika hali ya afya ya Watanzania. Kwa mfano, kumekuwa na maendeleo ya kuridhisha katika kupunguza viwango vya vifo vya watoto wachanga na watoto walio na umri chini ya miaka mitano. Hii imetokana hasa na uwekezaji zaidi katika udhibiti wa malaria na upatikanaji mzuri zaidi wa maji salama ya kunywa. Japokuwa kiwango cha maambukizi ya VVU/UKIMWI kinatofautiana kati ya mkoa mmoja na mwingine, kitaifa kiwango kimeshuka kutoka asilimia 5.7 hadi asilimia 5.1 katika miaka mitano iliyopita. Pamoja na kwamba maendeleo haya yanatia moyo, tatizo sugu la lishe duni (kudumaa) na viwango vya vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi vinaendelea kuwa vya juu, wanawake ndio wanaoathirika zaidi na VVU/UKIMWI. Takriban asilimia 60 ya watu wanaoishi na VVU ni wanawake.

Wakati Tanzania imepiga hatua nzuri katika kuandaa sera na mikakati ya kuendeleza uwezeshaji wa wanawake na usawa wa kijinsia, bado inayo safari ndefu katika utekelezaji wa sera hizo. Tanzania iko katika nafasi ya 47 kati ya nafasi 86 katika Kielelezo cha Taasisi za Kijamii na Jinsia cha mwaka 2012 (*Social Institutions and Gender Index*). Makisio ya Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu iliyoandaliwa na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) yanaiweka Tanzania katika nafasi ya 152 kati ya nchi 187. Tanzania iko katika nafasi ya 119 katika Kielelezo cha Kukosekana kwa Usawa wa Kijinsia (*Gender Inequality Index*) cha Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kati ya nchi 146, na nafasi ya 59 katika Kielelezo cha Tofauti za Kijinsia Kimataifa cha mwaka 2011 (*Global Gender Gap Index*). Yapo matukio mengi ya ndoa za utotoni nchini Tanzania huku umri wa kisheria wa kuolewa kwa wanawake ukiwa miaka 15 (au chini ya hapo, hadi miaka 14 kwa "ruhusa maalum"), wakati kwa wanaume ni miaka 18. Ndoa



# Tanzania imeweza kuvutia uwekezaji mkubwa wa kigeni.

za utotoni zinapelekea uwepo wa viwango vikubwa vya mimba za utotoni ambazo zinazuia uwezo wa watoto hao kumaliza shule na kupata ajira za maana. Uandikishaji wa watoto wa kiume na wa kike katika shule ya msingi karibu unalingana, lakini inapokuja kwenye viwango vya kumaliza shule ya sekondari hali sio nzuri sana. Viwango vya kumaliza shule ya sekondari kwa kundi la umri la miaka 20 hadi 24 vilikuwa asilimia 19.5 kwa wanawake na asilimia 32.7 kwa wanaume. Takwimu za mwaka 2010 za Utafiti wa Hali ya Afya ya Watu Tanzania (*Tanzania Demographic Health Survey*) zinaonyesha kwamba asilimia 20 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 20-24 hawakuwa na elimu kabisa, ukilinganisha na asilimia 9.6 ya wanaume. Pamoja na kwamba wanawake wanashika asilimia 36 ya viti Bungeni, wanawake kwa ujumla wao bado wanawakilisha asilimia 10 tu ya tabaka la wanasiasa wasomi katika ngazi ya wilaya na ngazi kwenda chini.

Katika masuala ya uchumi, Tanzania ilianza mageuzi ya kiuchumi katika miaka ya 80, na hadi leo ipo kwenye mpito unaokwenda taratibu kutoka ujamaa kuelekea mfumo wa soko huria. Katika muongo uliopita, Tanzania imeweza kuvutia uwekezaji mkubwa wa kigeni (Foreign Direct Investment - FDI) na imegundua gesi asilia siku za karibuni katika maeneo ya pwani, ambavyo kwa pamoja, vinaipa fursa ya kuongeza viwango vya ukuaji wa uchumi kwa kiasi kikubwa pale ambapo hifadhi za gesi hii zitakapoanza kutumika katika miaka saba hadi kumi ijayo. Hata hivyo, mazingira ya kibiashara bado yana changamoto nyingi. Ili kufikia lengo la kuwa nchi yenye kipato cha kati ifikapo mwaka 2025, ni lazima Tanzania iharakishe utekelezaji wa sera na taratibu ambazo zitavutia uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta muhimu za uzalishaji; lazima kudhibiti rushwa na ufisadi, kuandaa nguvu kazi yenye ujuzi na kuboresha miundombinu, hususan barabara na nishati. Vile vile, usalama duni wa wanyamapori, na kuongezeka kwa vitendo vya ujangili dhidi ya wanyapori muhimu (*keystone species*) kama vile tembo, vinadhoofisha sekta hii muhimu ya utalii na kuharibu urithi wa Bionuai yenye thamani ya kimataifa (*global biodiversity legacy*). Wakati huo huo, mabadiliko ya tabia nchi tayari yamesababisha: ongezeko la hali ya joto kwa nyuzi joto sentigredi moja, mabadiliko katika mfumo wa majira ya mvua, ongezeko la matukio ya hali ya hewa ambayo inazidi au kupungua kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na hali ya hewa ya wastani au ya kawaida (*extreme weather events*), na kuongezeka kwa kiwango cha maji kupita usawa wa bahari. Bila kupunguza uzalishaji wa gesiukaa kimataifa (*global greenhouse gas emissions*), mabadiliko haya ya tabia nchi yanatarajiwa kuendelea nchini Tanzania na kuleta athari mbalimbali katika afya ya binadamu, kilimo, mifugo, maji na mifumo ya ikolojia (hususan maeneo ya pwani na bahari, maeneo ya misitu ya mbugani na nyika). Mikakati ya maendeleo itahitaji kujikita katika kuimarisha uwezo wa kukabiliana na mazingira magumu yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi.

Ili kuweza kuunganisha fursa za kiuchumi zilizopo na kupunguza umaskini uliokithiri, Tanzania haina budi kuongeza ushirikiano wa kiuchumi katika ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwingineko. Pia ni lazima Tanzania ipanue masoko, ibuni njia ya kupunguza gharama za uzalishaji huku ikiongeza uwezo wa kuzalisha (*create economies of scale*), na kupunguza gharama za manunuzi au mauzo katika biashara za ndani kikanda na kimataifa. Chini ya uratibu wa Serikali ya Marekani na wafadhili wengine, USAID itaweka mkazo katika kupunguza vikwazo kwenye biashara na uwekezaji, na kuendeleza mauzo ya nje katika ukanda huu na kanda nyingine katika maeneo machache ya mnyororo wa thamani (*value chain*). Mkakati huu wa Ushirikiano wa Kimaendeleo utapunguza umaskini kwa kuwawezesha wanawake na vijana kuendeleza ukuaji jumuishi na mpana na kuboresha utawala wenye ufanisi.

# Mfumo wa Matokeo ya Mkakati wa Ushirikiano wa Kimaendeleo

## *(Results Framework)*:

Nadharia tete ya Mkakati huu wa Ushirikiano wa Kimaendeleo iliyoonyeshwa katika kielelezo Namba 1 cha Mfumo wa Matokeo katika ukurasa wa 9 inapendekeza kwamba USAID itaungana na wadau wa Kitanzania kutoka serikalini, asasi za kiraia (AZAKI), sekta binafsi, taasisi za serikali ya Marekani na wadau wengine wa kimataifa, kuisaidia Tanzania kuelekea hadhi ya nchi yenye kipato cha kati ifikapo 2025, kwa kutekeleza mambo matatu yafuatayo:

**Kuwawezesha Wanawake na Vijana**

Kwanza, ili kupunguza umaskini uliokithiri, kujenga jamii zilizo na afya bora zaidi, na kuendeleza ukuaji wa uchumi ulio jumuishi, ni lazima wanawake na vijana wa Kitanzania (ambao ni wananchi waliosahaulika kwa kiasi kikubwa na kutoendelezwa) waweze kumiliki rasimali na fursa muhimu za kujiletea maendeleo. Wanawake wakiwezeshwa kufikia uwezo wao kamili wa kuchangia katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii, kila mwanamke, watoto wake na jamii nzima kwa ujumla watafaidika na kustawi;


**Kufanikisha Ukuaji wa Uchumi ulio Jumuishi na Mpana**

Pili, ili kufanikisha na kuendeleza ukuaji wa uchumi ulio jumuishi na mpana, sekta muhimu zinazotegemea nguvu kazi shadidi ni lazima zikue kwa kasi kubwa zaidi, (yaani, kilimo na maliasili na utalii). Aidha, ni lazima kuondokana na vikwazo vinavyobana uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta hizi zinazotegemea nguvu kazi shadidi, hususan sekta ya umeme, ili kuhakikisha upatikanaji wa vyanzo vya uhakika vya umeme, na barabara za vijijini 'kutoka shambani kwenda sokoni' (*rural 'farm to market' roads*). Afua hizi na uwekezaji wa aina hii ndiyo njia ya kupunguza umaskini uliokithiri kwa idadi kubwa (asilimia 68) ya watu nchini ambao ni maskini.

**Kuimarisha Utawala Bora**

Tatu, kuimarisha uwezo wa serikali wa kutoa huduma bora pamoja na kuboresha ushiriki wa wananchi (*citizen engagement*) ni njia muhimu ya kufanikisha utawala ulio wazi, wa uwajibikaji na wa kidemokrasia pamoja na kuthibiti rushwa na kupunguza migogoro.

Malengo ya maendeleo na matokeo ya kati yaliyotolewa maelezo ya kina katika sehemu zinazofuata, kwa pamoja, yatafanikisha Lengo Kuu la Mkakati huu wa Ushirikiano wa Kimaendeleo.




*Kielelezo Na. 1: Mfumo wa Matokeo ya Mkakati wa Ushirikiano wa Kimaendeleo*

# Lengo la Kwanza la Maendeleo

## Wanawake na Vijana Wakitanzania wamewezeshwa

Nadharia tete chini ya lengo la 1 la maendeleo inatamka kwamba 'endapo wanawake na vijana watawezeshwa, watajenga familia na jamii zilizo na afya, watachangia ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Ukilinganisha wanawake na wanaume, wanawake wanatumia sehemu kubwa ya kipato chao kwa ajili ya mahitaji ya chakula, huduma ya afya, uboreshaji wa mazingira ya nyumbani, pamoja na kugharamia elimu ya familia zao, na hivyo kuleta mafanikio kwa watoto wao pamoja na kuchangia maendeleo ya muda mrefu ya kijamii na kiuchumi. Wanawake wakiwa na vipato vya juu na vya uhakika watawekeza katika elimu na afya, na hivyo kupelekea uwepo wa wananchi walioelimika zaidi na ambao wana uwezo wa kuchangia kikamilifu katika uchumi wa Tanzania. Vijana wanapaswa kusaidiwa kwa kupewa fursa za kuchangia katika kuleta mageuzi ya kijamii na kiuchumi Tanzania. Uzoefu wa kimataifa unaonyesha kwamba uwekezaji katika afya, lishe bora, elimu na stadi za kazi, hususan kwa wanawake na vijana, utawawezesha kuchagua njia za uzazi wa mpango wanazozitaka, kutokana na uelewa mzuri zaidi wa njia zilizopo (*informed family planning choices*).

Nchini Tanzania, wanawake wanaposhiriki katika maamuzi ya kifamilia na kisiasa na wanapokuwa na elimu bora na fursa pana zaidi za kuingiza kipato, wataweza kulea watoto wenye afya bora na elimu nzuri. Vivyo hivyo, kuwawezesha vijana kunaimarisha uwezo wa vijana kukidhi mahitaji yao binafsi ya kiuchumi na kuchangia ukuaji wa uchumi. Kwa upande mwingine, athari za kutowawezesha wanawake na vijana ni kubwa sana ikiwa ni pamoja na: watoto kuacha shule, afya duni, uchumi unayoyumba na jamii dhaifu isiyokuwa na mshikamano. Vyote hivyo vinapelekea uzalishaji mdogo zaidi na ukuaji wa uchumi wenye kasi ndogo. Japokuwa wanawake na vijana wanaunda kundi la watu wanaozalisha zaidi, ndilo kundi linaloathirika na mazingira magumu kuliko makundi mengine. Hivyo, kuwawezesha wanawake na vijana ni muhimu katika kuboresha maisha kijamii na kiuchumi nchini. Hata hivyo, wanawake na vijana wengi wa Kitanzania wana fursa chache tu za kupata huduma za afya, maji, lishe, elimu au fursa pana zaidi za kiuchumi; ikiwa ni pamoja na rasilimali zinazozalisha (*productive resources*) kama vile maji na ardhi pamoja na mikopo. Kwa kuongezea, athari za mab-

**Kuwawezesha wanawake na vijana ni muhimu katika kuboresha maisha kijamii na kiuchumi nchini.**

adiliko ya tabia nchi zinasababisha mazingira magumu ya kijamii na kiuchumi (*socio-economic vulnerability and adaptation*) ambazo zinaathiri zaidi wanawake ambao wanaunda sehemu kubwa ya watu maskini katika maeneo ya vijijini, walio na mbinu chache zaidi za kukabiliana na mazingira magumu na wenye wajibu mkubwa zaidi wa kuzalisha kiuchumi pamoja na kuzaa watoto. Kwa mfano, vyanzo vya maji vikikauka au kupungua kwa ubora, ni wanawake na watoto ndio wanaoathirika zaidi.

Uwezo wa wanawake na vijana kuendeleza maisha yao unakwazwa na sheria na tamaduni ambazo zinahalalisha vitendo vya kuwagandamiza na kuwaonea, ukilinganisha na makundi mengine. Kwa mfano, hapa Tanzania, viwango vya vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi ni vya juu wakati idadi ya wanawake wanaojiunga na sekondari na elimu ya juu iko chini. Ukizingatia kwamba kuna uhusiano kati ya kiwango cha elimu na umri ambao mtoto wa kike anazaa kwa mara ya kwanza, na kwamba uwezekano wa wasichana walio katika umri wa balehe kufa wakati wa kujifungua ni mkubwa zaidi, elimu inaweza kuwawezesha vijana kuchagua mbinu za uzazi wa mpango zinazofaa pamoja na kushiriki katika nguvu kazi. Tanzania ni nchi yenye viwango vikubwa vya uzazi. Wakati huo huo, watoto wengi zaidi walio na umri chini ya miaka mitano wanaendelea kuishi ukilinganisha na ilivyokuwa miaka kumi iliyopita.

Utafiti umeonyesha pia kwamba karibu ulimwenguni kote, elimu ni sharti muhimu katika kupunguza umaskini. Hata hivyo, kupata elimu peke yake haitoshi iwapo ubora na umuhimu wake ni hafifu ukilinganisha na mahitaji, au hali ya afya ya watoto ni duni. Kwa mfano, kudumaa kunaweza kupunguza uwezo wa watoto wa kutambua; VVU na UKIMWI katika kaya vinaweza kuwa kikwazo kwa mahudhurio ya darasani, pia kukosekana kwa usawa wa kijinsia kunaweza kupunguza uwezo wa wasichana kuhudhuria darasani na hivyo kuathiri ushiriki wao katika kukuza uchumi. Watu ambao ni maskini zaidi kuliko wengine na ambao wako pembezoni, wako katika mazingira magumu zaidi na mara nyingi hawatumii uwezo wao kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi.



# Lengo la Pili la Maendeleo

## Ukuaji wa uchumi ulio jumuishi na mpana umeendelezwa

Nadharia tete ya lengo la 2 la maendeleo inatamka kwamba iwapo sekta binafsi itawekeza katika nishati pamoja na sekta zinazotegemea nguvu kazi shadidi, kama vile kilimo, na maliasili na utalii, na iwapo wanawake na vijana wakipatiwa rasilimali na maarifa kuhusu namna ya kutumia fursa zilizopo katika sekta hizi, na kuwa na uhuru wa kuchagua ukubwa wa familia wanayoitaka, itawezekana kupunguza umaskini uliokithiri na kuendeleza kasi ya ukuaji ya uchumi jumuishi na mpana nchini Tanzania. LeMa2 litaharakisha ukuaji wa uchumi katika sekta za vijijini ambazo zinazalisha ajira (k.m. kilimo/uzalishaji na usindikaji wa vyakula na utalii uliojikita katika maliasili), litaondoa vikwazo katika uwekezaji wa sekta binafsi kwenye maeneo haya, na kuiweka Tanzania katika nafasi ambayo itapunguza mahitaji ya uzazi wa mpango ambayo hayajafikiwa. Vile vile, litasaidia kujenga mzunguko chanya na imara wa fursa za kiuchumi ambazo zitakua kwa kasi kubwa zaidi kuliko kasi ya ongozeko la idadi ya watu.

Kilimo pamoja na biashara ya kilimo vimeendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania, vinachangia takriban asilimia 28 ya Pato la Taifa, na kuajiri asilimia 77 ya idadi ya watu kitaifa. Tanzania imebarikiwa kuwa na utajiri wa maliasili ambao ukisimamiwa kwa njia endelevu, utakuwa msingi wa kilimo chenye manufaa. Hata hivyo, viwango vya sasa vya mavuno ya mazao ni asilimia 20-30 ya uwezo wa kuzalisha. Tanzania ikitumia msaada wenye malengo mahususi, kutekeleza sera na uwekezaji vinavyohakikisha umiliki wa ardhi na uhakika wa rasilimali (hasa kwa wanawake), kuboresha usambazaji wa pembejeo na minyororo ya thamani inayounganisha wakulima wadogo wadogo na masoko, pamoja na kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji, inaweza kupata ongezeko kubwa la kipato kutoka maeneo ya vijijini, hususan kwa wakulima wanawake na vijana. Kuongeza uzalishaji na faida itokanayo na kilimo ni jambo la msingi katika kupunguza umaskini na ukuaji wa uchumi nchini Tanzania.

Tanzania ina utajiri wa Bionuai yenye umuhimu wa kimataifa na ina mbuga za wanyamapori zinazostawisha sekta ya utalii na kuzalisha ajira kwa vijana na wanawake. Hata hivyo, sekta hii inatishiwa na hali ya hatari ya ongezeko la vitendo vya ujangili uliokithiri (unaolenga wanyapori muhimu, kama vile tembo na vifaru), pamoja na usimamizi na uhifadhi mbovu wa maeneo muhimu ya Bionuai. Usimamizi bora hapa nchini wa maeneo yenye maliasili za kudumu kwa kuzaana au kujirudia tena na tena (*country's renewable natural resource base*) na huduma zitokanazo na maliasili hizo, ikiwa ni pamoja na maeneo yaliyotengwa na jamii kwa ajili ya hifadhi yawanyamapori (*Wildlife Management Areas*), unaweza kuendeleza na kukuza sekta ya utalii.

Umaskini wa Tanzania unadhihirishwa na uchumi ulioshindwa kukua sambamba na kasi ya ongezeko la idadi ya watu nchini. Kiwango cha uzazi cha mwaka 2010 ni watoto 5.4 kwa kila mwanamke na mahitaji ya uzazi wa mpango yasiyofikiwa nchini Tanzania kwa sasa ni asilimia 25. Upo uwezekano wa mahitaji haya yasiyofikiwa kuongezeka jinsi wanawake na vijana wanavyozidi kuwezeshwa (LeMa 1) na kuwa na uwezo wa kuzalisha (LeMa 2). Kufanikisha matarajio ya Tanzania ya kuwa na uzazi wa mpango kutaisaidia nchi kufikia lengo la kuwa nchi yenye kipato cha kati, kwa kupunguza shinikizo litakalotokana na ongezeko la idadi ya watu katika mifumo ya utoaji huduma na maeneo ya vyanzo muhimu vya maliasili.

[2] *Hii ni asilimia ya wanawake ambao hawataki kupata ujauzito (aidha, hawapendi kuzaa tena au wanataka kuahirisha ujauzito unaofuata kwa angalau miaka miwili), lakini hawatumii njia za uzazi wa mpango.*



# Lengo la Tatu la Maendeleo

## Utawala wa kidemokrasia umeimarishwa

Nadharia tete chini ya lengo la 3 la maendeleo inahusu kuondoa vikwazo vya msingi vinavyokwamisha utawala bora na huduma kwa umma. Nadharia hiyo inatamka kwamba wananchi wanapoiwajibisha serikali yao, wanakuwa na imani zaidi kwamba serikali itakidhi mahitaji yao na watakuwa na ari ya kushiriki kikamilifu kuchangia rasilimali zao wenyewe na kutoa ushirikiano. Vile vile, wabia wa maendeleo wanaweza kuwekeza rasilimali zao kwenye maendeleo ya kijamii na kiuchumi imani yao katika mifumo ya nchi inapoongezeka. Msisitizo wa lengo la 3 ni kuhakikisha kwamba wanawake na vijana wanakuwa na sauti katika maamuzi mbalimbali na kushiriki kikamilifu katika kuleta maendeleo, mageuzi na utawala bora.

USAID itasaidia kuendeleza utawala bora, uwazi na uwajibikaji; itasaidia taasisi za serikali kuu na za serikali za mitaa ambazo zinahamasisha uwajibikaji na kuimarisha utoaji wa huduma kwa umma; na itawekeza katika ngazi ya halmashauri (na huenda hata ngazi ya mkoa) ili kuiongezea serikali uwezo wa kupanga na kutoa huduma kwa wananchi wake. Kwa ushirikiano wa karibu na Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania, USAID itasaidia kuiongezea Serikali ya Tanzania uwezo wa kugharamia huduma za afya kwa ajili ya wananchi wake na kuwezesha ukusanyaji wa raslimali za ndani (*Domestic Resource Mobilization*). Hii ni pamoja na kutumia vigezo mbalimbali vya kupima ufanisi wa utoaji wa huduma katika ngazi ya kituo cha kutolea huduma, ambapo vituo vitakavyoonyesha utendaji bora vitatunukiwa rasilimali-fedha zaidi chini ya mpango wa ufadhili unaozingatia mafanikio ya utendaji (*Results-Based Financing*). USAID itazisaidia asasi zisizo za kiserkali (*non-governmental organizations*) na AZAKI kuwa mawakala wa mabadiliko wenye uwezo wa kujiendesha wenyewe (*fully-fledged and self-sustaining agents of change*). Katika maeneo yote hayo, wanawake na vijana watakuwa walengwa mahsusi. USAID itatathmini na kusaidia kufuatilia maeneo yenye dalili ya kutokea migogoro (*flashpoints*) ili kuisaidia Tanzania kuendeleza hali ya utulivu iliyopo nchini.



# Matokeo Mtambuka ya Muda wa Kati

## Maamuzi, mipango na utekelezaji kwa kutumia takwimu vimeboreshwa

USAID ina mamlaka ya kutekeleza miradi ya maendeleo yanayoendana na taratibu zake za kutumia ushahidi wa matokeo (*evidence-based approach to development*). Kutokana na utaratibu huo, USAID/Tanzania itaunga mkono juhudi za nje na za ndani kukusanya, kusambaza, kuchambua, na kutumia takwimu kwa ajili ya kutoa taarifa na kuongoza utekelezaji wa mafanikio wa mipango ya maendeleo. Juhudi hii inaihusisha USAID/Tanzania na washirika wake wa kutekeleza miradi (*implementing partners*) na, muhimu zaidi, taasisi za serikali na vikundi vya kiraia. Upatikanaji wa takwimu zilizo sahihi, bora na za wazi hapa Tanzania, unakabiliwa na vikwazo vikubwa ikiwa ni pamoja na: mapengo ya takwimu za viashiria vya kijamii na kiuchumi vinavyohitajika kufuatilia mafanikio ya sera na mipango ya maendeleo, uratibu hafifu, ufahamu mdogo na matumizi yasiyotosheleza ya takwimu nchini; pamoja na watu walio katika nafasi za kufanya maamuzi kutozipa takwimu hizi kipaumbele stahiki. Katika kushughulikia changamoto hizi, Serikali ya Tanzania iliandaa Mpango wa Taifa wa Uandaaji wa Takwimu (*National Plan for Development of Statistics*), ambao unajulikana pia kama Mpango Mkuu wa Takwimu Tanzania (MMTATA: 2009/2010 – 2013/2014) (Tanzania Statistical Master Plan – TSMP). Kwa kuwa Serikali ya Tanzania, sekta binafsi, AZAKI na wabia wa maendeleo wanahitaji kipimo kisicho na utata na kilicho rahisi (*clear, unambiguous and systematic measurement and reporting*) kwa ajili ya kupima na kutoa taarifa kuhusu mafanikio yaliyopatikana, MMTATA unalenga kusaidia uaandaji wa sera na kuwezesha utoaji wa maamuzi kwa kuzingatia ushahidi wa mafanikio ili maamuzi ya wadau yawe yanafanyika kwa kutumia takwimu za kuaminika na zilizo sahihi. Programu zinazotekelezwa na USAID/Tanzania zinazingatia na kutumia matokeo yenye ushahidi thabiti. Hata hivyo, USAID inaweza kufanya vizuri zaidi katika hili.

**Wananchi wanapoiwajibisha serikali yao, wanakuwa na imani zaidi na kutoa ushirikiano.**

# Usimamizi wa Utekelezaji wa Mkakati wa Ushirikiano wa Kimaendeleo

Mkakati huu wa Ushirikiano wa Kimaendeleo umeandaliwa kwa ushirikiano kati ya USAID/Tanzania, Serikali ya Tanzania na wabia wake, wajumbe kutoka AZAKI Tanzania, sekta binafsi, na wafadhili wengine hapa nchini. Mkakati huu uliandaliwa katika kipindi cha miaka miwili ya mazungumzo, majadiliano na uchambuzi. Chambuzi zilizotumika kuandaa Mkakati huu, zinajumuisha utafiti uliofanywa na wataalamu wa hapa nchini na wa kimataifa, ambao walichambua fursa na changamoto zilizopo katika uandaaji wa programu za maendeleo nchini Tanzania kwa kuzingatia vigezo vya usawa wa kijinsia, hifadhi ya mazingira na uendelevu wa miradi.

USAID hutekeleza mipango yake ya maendeleo kwa kutoa ruzuku, na kufanya mikataba na washirika wake wa utekelezaji yakiwemo makampuni ya kimataifa na ya Kitanzania, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, au taasisi za kiserikali. USAID inaweka kipaumbele zaidi kwenye utoaji wa msaada wa kifedha moja kwa moja kwa taasisi za Kitanzania (ama za kiserikali au zisizo za kiserikali) ili kupata mafanikio, kuimarisha uwezo wa ndani, na kuongeza uwezo wa taasisi kuendeleza miradi.

Ili kufahamu kama tumefanikiwa malengo yetu, USAID na washirika wake iliweka vipimo na kuandaa vigezo vya wazi vya kutathmini maendeleo ya utekelezaji, kwa kutumia vipimo na vigezo hivyo. Chini ya Mkakati huu wa Ushirikiano wa Kimaendeleo, vipo viashiria vya kupima utekelezaji wa kila lengo la maendeleo na matokeo ya kati, vilivyoelezwa kwa ufasaha, vinavyotumia njia za upimaji wa matokeo zilizo wazi na malengo ambayo yameainishwa chini ya Mpango wa Ufuatiliaji wa Utendaji (MUU) wa Mkakati huu wa Ushirikiano wa Kimaendeleo. Utoaji wa taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa mpango huu zinafuatilia matokeo dhidi ya malengo yaliyowekwa na kusaidia kufanya maamuzi kuhusu utekelezaji.

Mbali na MUU, kwa mara ya kwanza katika miaka zaidi ya 50 ya ushirikiano baina ya Tanzania na Marekani, USAID/Tanzania imeunda jopo la wataalamu wa Kitanzania kusaidia kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa Mkakati huu wa Ushirikiano wa Kimaendeleo. Kikundi hiki kijulikanacho kama 'Kikundi cha Ushauri' cha Mkakati wa Nchi wa Ushirikiano wa Kimaendeleo, kimeundwa na wataalamu wa Kitanzania waliobobea katika masuala ya maendeleo kutoka serikalini, AZAKI, mashirika ya ufadhili na sekta binafsi. Kikundi hiki cha ushauri kitatoa mawazo na kuishauri USAID kuhusu maendeleo katika ufanikishaji wa matokeo ya Mkakati huu wa Ushirikiano wa Kimaendeleo. Kwa mantiki hiyo, kikundi hiki cha Ushauri kitakuwa na ufahamu wa kina kuhusu kazi za USAID Tanzania katika vipengele vyote vya Mfumo wa Matokeo wa Mkakati wa Nchi wa Ushirikiano wa Kimaendeleo, na kitakutana angalau mara moja kwa mwaka kupitia maendeleo ya utekelezaji na kuishauri USAID kuhusu namna ya kuharakisha na kuboresha ufanikishaji wa matokeo na kuimarisha ushirikiano.

Mkakati wa Nchi wa Ushirikiano wa Kimaendeleo ni mkakati utakaojumuisha mapitio ya mara kwa mara ili kuhakikisha matokeo tarajiwa yanapatikana (*iterative strategy*). Katika kipindi chote cha utekelezaji wa mkakati huu, USAID itafuatilia kwa uangalifu na umakini mkubwa mafanikio/matokeo ya utekelezaji wake. Vile vile, itapitia mabadiliko katika muktadha na hali ya dhana zote muhimu katika ngazi zote za mfumo wa matokeo ya Mkakati huu nchini Tanzania, ikilenga zaidi kwenye athari katika ufanikishaji wa matokeo. Mapitio ya Mkakati yatafanyika kila mwaka, na patakuwa na mapitio mapana (*comprehensive review*) angalau mara moja katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mkakati. Mapitio mapana yatajumuisha mazungumzo na wabia, wadau na wafadhili wengine, na yanaweza kupelekea marekebisho katika matokeo, mitazamo na/au mfumo wa matokeo (*CDCS results, approaches, and/or results framework*) ya Mkakati wa Nchi wa Ushirikiano wa Kimaendeleo.

Kikundi cha Ushauri cha Mkakati wa Nchi wa Ushirikiano wa Kimaendeleo kitakuwa na wajibu mkubwa wakati wa mapitio ya kila mwaka na mapitio mapana. Mapitio yote yatalenga zaidi kuangalia mabadiliko katika Mkakati wa Maendeleo wa Serikali ya Tanzania ili kuhakikisha kwamba Mkakati wa Nchi wa Ushirikiano wa Kimaendeleo unafungamana/unaendana na vipaumbele vya maendeleo vya Tanzania pamoja na vile vya wafadhili wengine na kwamba panakuwa na uwajibikaji wa pamoja. Aidha, mapitio yatasaidia kuimarisha msaada wa Tanzania katika kuhakikisha kuwa Mkakati wa Nchi wa Ushirikiano wa Kimaendeleo unafanikiwa na kuongeza uwezekano wa matokeo ya Mkakati huu kuwa endelevu.



**SHIRIKA LA MAREKANI LA MISAADA YA MAENDELEO YA KIMATAIFA**
Jengo Na. 686 Barabara ya Zamani ya Bagamoyo, Msasani
S.L.P. 9130
Dar es Salaam, Tanzania

www.facebook.com/usaid.tanzania
www.usaid.gov/tanzania

**SHIRIKA LA MAREKANI LA MISAADA YA MAENDELEO YA KIMATAIFA**
Jengo Na. 686 Barabara ya Zamani ya Bagamoyo, Msasani
S.L.P. 9130
Dar es Salaam, Tanzania

www.facebook.com/usaid.tanzania
www.usaid.gov/tanzania